Kwa kushirikiana na familia na jamii zao, tunatetea usalama, udumishaji na afya ya kila mtoto tunatoa huduma kwa njia inayoheshimu familia na mila.

Huduma za
Watoto za
Franklin Couty

855 West Mound Street
Columbus, Ohio 43223-2208
614-275-2571
614-275-2755 (faksi)
www.childrenservices.franklincountyohio.gov/

Franklin County Children Services
Protecting Children by Strengthening Families

*"Kulinda Watoto kwa Kuimarisha Familia"*

Ilmechapishwa na Huduma za Watoto za Franklin County
Ofisi ya Haki za Mteja
**CS-Consumer Rights Book–English (Rev. 4-2017)**



Franklin County Children Services
Protecting Children by Strengthening Families

# Haki za Mtumiaji & Ufahamu

______________________________________

**Jina la mfanyikazi na simu:**

______________________________________

**Msimamizi:**

______________________________________

**Mkurugenzi Msaidizi:**

______________________________________

**Mkurugenzi:**

Ofisi Ilipo:

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| Usajili | …… | 4071 E. Main St. | …… | 614.229.7100 |
| Mashariki | …… | 4071 E. Main St. | …… | 614.421.5500 |
| Magharibi | …… | 1919 Frank Rd. | …… | 614.278.5800 |
| Idara ya Kutwaa. | …… | 855 W. Mound St. | …… | 614.341.6000 |
| Idara ya Mafunzo. | …… | 855 W. Mound St. | …… | 614.278.5906 |
| Rasilimali za Watu | …… | 855 W. Mound St. | …… | 614.351.2000 |
| Haki za Wateja | …… | 855 W. Mound St. | …… | 614.275.2621 |

**Ofisi za Usimamizi**
855 West Mound St.
Columbus, OH 43223
614-275-2571

24-Hour Hotline
614-229-7000

Kupitia ushiriano wa familia na jamii zao, tunatetea usalama udumishaji na uzima wa kila mtoto tunayemhudumia kwa njia inayoheshimu familia na utamaduni.

## Kuhusu kijitabu hiki

Ni sera yetu kukupa kijitabu hiki na kukijadili katika mahojiano ya ki-binafsi ukiwa pamoja na mmoja wa wafanyikazi wetu. Ikiwa una maswali, tafadhali wasiliana na mhudumu wako au msimamizi aliyeandikwa kwenye jalada. Ikiwa kesi yako imefunguliwa na kutumwa kwa mojawapo ya ofisi zetu za mashinani, mhudumu wako mpya atahakikisha kwamba una nakala yako ikiwa na majina ya msimamizi na mhudumu wako mpya.

## Kuhusu haki yako ya kujieleza vyema

Watu wote ambao hawawezi kujieleza kwa Kiingereza, iwe kusoma au kuandika , watapata huduma kwa usawa zinazopeanwa na Huduma za Watoto za Frankline County.Maelezo yanayofaa yatapeanwa kupitia wahuduma wa idara ya watoto ikiwezekana.Isipowezekana, mtafsiri aliyehitimu atapeanwa bila malipo.

**Yaliyomo**

**Huduma kwa watoto za Frankline Kaunti ni nini?** ········3

**Ninaweza tarajia nini kutoka kwa FCCS?** ········4

**Ni vipi Sheria ya Maslahi ya Watoto itakuathiri?** ········5

**Ni huduma zipi zinazoweza kusaidia kusaidia familia yangu?** ········6

**Nini kinafanyika ikiwa watoto wangu lazima watoke nyumbani?** ········7

**Haki zangu ni zipi?** ········8

**Haki zangu zimelindwa vipi?** ········12

**Wakati janga linapotukia** ········15

*Ilirekebishwa Aprili 1, 2017*



## Maandishi

## Maandishi



## Je, huduma za watoto za Franklin county ni nini?

Shirika letu limejukumiwa na sheria kuchunguza dhuluma za watoto, kutelekezwa na kesi za utegemezi. Tutahusika tu kuhakikisha usalama kwa watoto au kusaidia familia wakati wa janga.Lengo letu la kimsingi ni kuwaweka watoto salama pale nyumbani na kupeana zile huduma ambazo zinaweza kuzuia kesi isifunguliwe. Kesi ikifunguliwa, tutahusika kwa njia tatu. Ikiwa motto anaweza kudumishwa nyumbani, tutashirikiana na hio familia katika mpango uliokubalianwa ili kusuluhisha shida iliyowaleta kwetu.Mara nyingine ni muhimu kuwaondoa watoto kutoka manyumbani mwao.Ikidhibitika kuwa haiwezekani kuwapatanisha mtoto na familia shirika litatafuta ulinzi wa kudumu na kuwapeana waweze kutwaliwa.

Wakati wowote kesi ingalipo, familia zinahimizwa kupeana mchango wao na wawe sehemu ya timu inayofanya maamuzi. Familia zinahudumiwa vyema zaidi wakati zinasaidia kutambua maswala ambayo yanawachanga na wanahusishwa katika uundaji mpango wa huduma wa kuwasaidia.

Kila mtoto anastahili kupata boma thabiti,na ya kudumu.Kudumu huku kunawezachukua hali tofauti- kupatanishwa na familia alikozaliwa, utunzi na familia, mawasiliano na familia lezi na /au mawasiliano na jamii yote yanaweza kupeana usaidizi wa kudumu maishani.

**24-Hour Hotline614-229-7000**

**Huduma za watoto zinataka upige simu ikiwa:**

- ☎ Unadhania huduma za ulinzi zinaweza kuwa za msaada kwako ama familia yako.
- ☎ Ulipokea huduma za ulinzi hapo awali lakini unazihitaji tena.
- ☎ Unadhania mtoto yeyote ama familia inahitaji huduma za ulinzi.

-Mpigaji simu ana haki ya kutotambuliwa.-

**Huduma za watoto hufuata kanuni hizi za kimsingi:**

- ♦ Sisi ni wataalamu wa masilahi ya watoto;
- ♦ Tunaheshimu familia;
- ♦ Tunathamini kila mtoto; na
- ♦ Tunathamini ushirikiano

## Ninaweza kutarajia nini kutoka kwa huduma za watoto?

Wafanyikazi wetu hufanya kazi na familia ili kusuluhisha shida zao. Sheria inahitaji huduma za watoto kuchunguza madai kuhusu watoto ambao wanaweza kuwa wamedhulumiwa, kutelekezwa au wategemezi na wanahitaji ulinzi.

**Simu hizi mara nyigi zinahusu:**

- Kukosa utunzi, chakula, makao, bidhaa za matumizi, matibabu kwa mtoto
- dhuluma mwilini wa mtoto
- dhuluma ya mtoto kingono
- Mtoto anayekosa kuboreka, kukua na kuendelea
- Utelekezi wa kimasomo
- Mtoto anayeonyesha shida mbaya za kitabia
- Mtoto ambaye ametoroka kutoka nyumbani
- matumizi ya mihadarati au pombe katika familia
- usalama au ulinzi wa mtoto
- kifo cha mtoto

Mfanyikazi a huduma za watoto atakueleza ni maswala gani nyeti yaliripotiwa na kutaka kujua ikiwa kuna shida katika swala lolote.Hii itafanywa kwa kuzungumza nawe, wanao, shule,mtaalamu, na wengine wanaohusika, ikibidi.Katika sheria ya Ohio, jina la mtu aliyeripoti **linabanwa** na haliwezi kufichuliwa.

Ikiwa kweli kutokana na ule uchunguzi zinaonyesha kuwa hakuna hitaji la ulinzi, tutakueleza, na uchunguzi utakoma.

Ikiwa zile kweli zinaonyesha kuwa kuna hitaji la kiulinzi, Huduma za watoto itafanya kazi nawe. Kazi hii inaweza kufanywa kupitia maelewano, au amri kutoka kwa korti la watoto.

Mpango wa kesi utaundwa kwa msaada wako na huduma muhimu zitajumlishwa katika mpango wa kesi. Mpango huu unaeleza kile mzazi, mtoto na/au shirika litafanya ili kufanya mabadiliko yanayofaa. Mahitaji yako au yale ya wanao yanapobadilika, ule mpango unaweza kubadilishwa. Utaulizwa utie sahihi mpango huu na mabadiliko yoyote uliyofanyiwa. Utapata nakala ya mpango wa kesi.

Mikutano ya kesi yako inafanya kwa mara isiyopungua mbili na Huduma za Watoto ( na Korti la watoto linapohusika) kuusasisha mpango ule na kuangazia maendeleo yaliyoafikiwa. Ikiwa familia yako haikubaliani na huduma au uamuzi, hatua zafaa kuchukuliwa ili kushughulikia hayo maswala.



## Mawasiliano

**Jina:** ____________________

**Anwani:** ____________________

**Jiji, Jimbo,namba ya posta:** ____________________

**Simu/ Barua Pepe:** ____________________

**Jina:** ____________________

**Anwani:** ____________________

**Jiji, Jimbo,namba ya posta:** ____________________

**Simu/ Barua Pepe:** ____________________

**Jina:** ____________________

**Anwani:** ____________________

**Jiji, Jimbo,namba ya posta:** ____________________

**Simu/ Barua Pepe:** ____________________

**Jina:** ____________________

**Anwani:** ____________________

**Jiji, Jimbo,namba ya posta:** ____________________

**Simu/ Barua Pepe:** ____________________

## Mawasiliano

**Jina:** ______________________________

**Anwani:** ______________________________

**Jiji, Jimbo,namba ya posta:** ______________________________

**Simu/ Barua Pepe:** ______________________________

**Jina:** ______________________________

**Anwani:** ______________________________

**Jiji, Jimbo,namba ya posta:** ______________________________

**Simu/ Barua Pepe:** ______________________________

**Jina:** ______________________________

**Anwani:** ______________________________

**Jiji, Jimbo,namba ya posta:** ______________________________

**Simu/ Barua Pepe:** ______________________________

**Jina:** ______________________________

**Anwani:** ______________________________

**Jiji, Jimbo,namba ya posta:** ______________________________

**Simu/ Barua Pepe:** ______________________________



**Ripota aliyeagizwa anayeripoti ya dhuluma kwa mtoto au utelekezi. Kufuatia ombi, ripota ataelezwa yote yafutayo:**

- Ikiwa PCSA imeazisha uchunguzi.
- Ikiwa PCSA inaendelea na uchunguzi.
- Ikiwa PSCA inahusika na mtoto kwa vyovyote vingine ambaye ndiye kiini cha ripoti ile.
- Hali ya afya kwa jumla ya yule mtoto ambaye ndiye kiini cha ile ripoti.
- Ikiwa ile ripoti imesababisha malalamishi kuwekwa kufanywa katika korti la watoto au kwa mashtaka ya uhalifu katika korti nyingine.

**Sheria ya Masilahi ya Watoto ya India** (ICWA) ni sheria ya kitaifa inayoazimia kuweka watoto wa Kihindi wa America pamoja na familia za Kihindi za Amerika. Bunge lilipitisha ICWA mwaka wa 1978 kufuatia watoto wengi wa kihindi kutolewa nyumbani kwao na mashirika ya umma na yale ya kibinafsi.Nia ya bung e chini ya ICWA ilikuwa "kulinda masilahi ya watoto wa kihindi na kutetea udhabiti na ulinzi wa makabila ya Kihindi na familia zao" (25 U.S.C. & 1902). Wafanyikazi lazima waangazie mambo kadhaa wanaposhulikia kesi ya ICWA ikiwemo:

- kutoa "juhudi hai" kwa ile familia;
- kutambua mahali panapofaa chini ya masharti ya ICWA;
- kueleza kabila la mtoto na wazazi wa mtoto kuhusu kesi ya mtoto; na
- kufanyajuhudi ili kuhusisha kabila la mtoto na wazazi wake katika ile kesi.

Anayeshughulikia kesi yako atakueleza haki zako chini ya ICWA na mambo mengine ya kesi katika njia rahisi unayoweza kuelewa.

Ukihisi kuwa ICWA haifanyishwi kazi vyema katika kesi ya mwanao, unafaa kuzungumza na msimamizi wa huyo mhudumu wa kesi. Ofisi ya Haki za Mteja pia inaweza kusaidia kwa kukuhakikishia kuwa ICWA inafuatwa.

## Ni huduma zipi zinazoweza kusaidia familia yangu?

**Huduma za Watoto hutoa huduma ikiwemo:**

- uchuguzi wa dhuluma kwa mtoto na utelekezi
- huduma za ulinzi na kushughulikia kesi
- huduma kwa wanaobaleghe
- huduma za ushauri
- huduma za ki-nyumbani
- huduma za mpango wa nyumbani
- huduma za kujitolea
- huduma za kiafya kwa watoto
- huduma za kuishi huru kwa wanarika wa mika 16 na kuendelea
- huduma za kutwaa watoto wa rika zote
- huduma za udumishaji wa familia

**Huduma za watoto huripoti kwa mashirika ya kijamii kwa huduma zingine za msaada:**

- huduma za afya ya akili
- mafunzo ya malezi
- tathmini ya kiakili/mashauriano
- tathmini na matibabu ya utumiaji wa mihadarati na pombe
- kuwasaidia watoto mchana
- huduma za kusaidia makuzi bora ya watoto
- msaada wa vifaa
- nyumba
- huduma za wanaobaleghe walio na matatizo



**Ikiwa FCCS inafanya kazi nawe na familia yako janga linapotukia…**

Ikiwa janga hilo **linakuathiri pamoja** na familia na linahitaji uhamisho wa dharura wa familia yako kutoka nyumbani au walipo, tafadhali eleza FCCS mara moja kwa 614-229-7100. Tafadhali kuwa tayari kutoa habari za kutosha ili kutuwezesha kukutambua na mahali utakapokuwa unaishi.

Ikiwa janga **linaathiri jamii yote**, tafadhali sikiliza vyombo vya habari kwa mawasiliano kutoka FCCS.

Ikiwa janga **linaathiri kutembelewa** na wanao au ikiwa tembeleo lako limeamriwa na korti, tafadhali tujulishe na tutafanya kazi nawe ili matembezi yako yasiathirike wakati huu mgumu.

Wakati wa hali mbaya ya hewa, uamuzi wa kukatiza matembezi na usafiri utaingiana na ule Mfumo wa Dharura wa Viwango vya Theluji. Matembezi yatakatizwa ikiwa kuna kiwango cha Theluji cha 2 au 3// Dharura ikipeanwa kwa:

- Franklin County
- Kaunti anakoishi mtoto
- Kaunti ya matembezi
- Kaunti yoyote msafirishaji atakayopitia

Ikiwa hivi, tafadhali wasiliana na Usaidizi wa Matembezi kwa 614-229-7001 wakati wa dharura hii ya kianga. Juhudi za kutosha zitafanywa ili kulipisha matembezi yoyote yaliyokatizwa wakati hali ya anga itaruhusu.

Juu ya harakati ya malalamishi ya Huduma za Watoto, Idara ya Ohio ya Kazi na Huduma za Familia ina wajibu wa kuhakikisha mashirika yote ya huduma  za watoto ya kaunti  yamefuata sheria. Unaweza kuwasiliana nao kwa kupigia , Idara ya Ohio ya Kazi na Huduma za Familia, isiyolipishwa kwa 866-886-3537 Chaguo la 4.

Huduma za Watoto zinadai kurejeshewa kwa ajili ya huduma kwa watoto chini ya programu za kitaifa na inahitajika na sheria kutoa huduma kulingana na taratibu za Kitaifa.

Ikiwa unaamini kwamba umetengwa kwa misingi ya rangi, kitaifa, ulemavu wa kimwili au kiakili, jinsia au umetengwa vinginevyo chini ya programu  yoyote, huduma au manufaa yaliyoidhinishwa na kutolewa na Huduma za Watoto za Franklin County unaweza kuwasiliana na huduma zifuatazo:

- Huduma za Watoto za Franklin County, Mratibu wa Haki za Raia (CRC) ni mtaalamu wa kushughulikia lalama kuhusu kutengwa. CRC anaweza kusaidia au kushauri kwa maswala yanayohusu haki za raia. CRC ipo 855 West Mound St, Columbus, OH, 43223, na atafikiwa kwa 614.275.2621;
- Huduma ya Haki za Kisheria ya Ohio, 8 E. Long St, 5th Floor, Columbus, Ohio 43215-2999, State-wide toll-free (voice): 800-282-9181, State-wide toll-free(T.T.Y.): 800.858.3542, Nambari ya simu: 614.466.7264; T.T.Y.: 614.728.2553, Faksi: 614.644.1888; na
- Afisa wa Haki za Raia, U.S. Dept. of Health and Human Services, 200 Independence Ave, S.W., Rm. 509F, HHH Bldg., Washington, D.C. 20201, toll-free TDD line: 800.537.7697

**Ikiwa unahisi unahisi ulistahili huduma ambazo hukupewa unaweza kutuma malalamishi kwa mojawapo ya mashirika kadhaa kama vile, na bila kufungia:**

**State of Ohio Counselor, Social Worker and Marriage & Family Therapists Board,**
77 South High Street,24th floor
Columbus, Ohio 43215
614-466-0912

**State Board of Ohio Psychology,**
77 South High Street, Suite 1830
ColumbusOhio 43215
614-466-8808

**Alcohol, Drug Addiction and Mental Health(ADAMH)Services**
447 E. Broad St.
Columbus, OH 43215
614-224-1057

**State of Ohio Nursing Board**
17 S. High St., Suite 400,
Columbus, Ohio 43215
614-466-3947



## Ni nini kinafanyika ikiwa wanangu inabidi watoke nyumbani?

**Watoto wote wanastahili makao ya kudumu.Katika juhudi za kuhahakikisha hili, wanaweza kuwekwa kwa muda katika mazingira yanayokaribia kufanana na nyumbani kabisa. Mazingira haya hujumlisha:**

- makao kwa mtu wa familia- ya ukoo.
- makao ya malezi
- makao ya jumla
- makaazi yaliyo karibu na nyumbani inavyowezekana
- Makao ya malezi

**Familia yako inatarajiwa kufanya kazi kama mshirika wa Huduma za Watoto ili kuwatia nguvu na kawapatanisha. Hii hufanyika ili kuwapa watoto udumishaji.**

**Familia zinatarajiwa ku:**

- kusaidia kuandika mpango wa kesi unaojumlisha huduma za kushughulikia mahitaji ya familia yako;
- kupeana makao safi, salama na yenye upendo kwa mtoto au watoto wako;
- kukutana na mhudumu wako na wafanyikazi wengine kuangazia kunavyoendelea;
- kuhudhuria na uhusike katika program huduma zilizoandikwa kwenye kesi//mpango; na
- kuhudhuria vikao vya korti na kufuata amri za korti zilizowekwa na korti.

Wakati woto watoto wakija kuhudumiwa, Huduma za **Watoto hueleza idara ya kazi na huduma za familia ya Kaunti ya Franklin na Shirika la Utekelezaji wa msaada kwa Watoto la Kaunti ya Franklin.**

Muulize mhudumu wako akupe nakala ya kijitabu "**Mbali na Nyumbani, Mpaka Nyumbani**". Kina maelezo ya harakati ya uunganishaji na maswali yanayoulizwa sana. Kila  wa miaka 14 na zaidi atapokea "**Kijitabu cha Haki za Vijana wa malezi badala**" kuhakikisha kwamba mtoto anajua haki zake zinazohusu elimu, afya, kutembelewa na kushiriki kortini akiwa katika malezi badala.

## Haki zangu ni zipi?

Huduma za watoto imejitolea kudumisha mazingira huru yasiyo na dhuluma wala mateso na haitayavumilia hayo yakifanyiwa mtu kwa ajili ya rangi yake, dini, kanuni ya imani, rangi, taifa analotoka,jinsia, ikiwa ameoa au la, umri, ulemavu wa kimwili au kiakili, msimamo wa kujamii, hali ya kijeshi, msimamo wa kisiasa, umemba wa kikundi, au matendo ya kisheria.

Sheria za Ohio na za kitaifa zinapeana ulinzi maalum wa haki zako unapokuwa ukipokea huduma za Huduma za watoto za Franklin Kaunti. Maswali zaidi kuhusu haki zako yanaweza kujadiliwa pamoja na wahudumu au yeyote katika Ofisi ya Haki za Mteja.

Ofisi ya Haki za Mteja ya Huduma za Watoto imeweka utaratibu wa kuangazia malalamishi ya mteja na rufaa za usimamizi. Ofisi ya Haki za Mteja huwafahamisha wateja kuhusu haki zao chini ya sera ya mashirika na sheria za Ohio. Ofisi ya Haki za Mteja inawajibika kwa kuhakikisha ufuataji wa sheria wa mashirika kwa haki za mteja na malalamishi/sheria za harakati ya kukata rufaa. Waliohitimu kupata harakati ya malamishi/kukata rufaa ni,na haijawafungia,watoto, wazazi,walezi wa ukoo na wasio wa ukoo,watu binafsi walioshukiwa kumdhulumu au kumtesa mtoto, na wataalam walio na jukumu katika huduma zinazotolewa na wafanyikazi. Ofisi ya Haki za Mteja:

- Hufanya kazi kama mwelekezi wa awali wa malalamishi;
- Hufanya kazi kama afisa msikilizi katika matokeo ya uchunguzi wa yanayozozaniwa;
- Hufanya kazi kama mratibu wa haki za raia;
- Hufanya kazi kama wakala wa uhakiki;
- Hupeleka ripoti kwa bodi;
- Huripoti kwa mkurugenzi mtendaji kwa ajili ya maswala ya bajeti na usimamizi. Majadiliano kuhusu kesi binafsi na mkurugenzi mtendaji zinaripotiwa kwa mwenyekiti wa bodi kwa maandishi; Haiwezi kuchukuliwa hatua za kinidhamu bila idhini ya mwenyekiti wa bodi; na
- Inaweza kuomba makao katika ajenda ya bodi wakati wowote ili kuripoti kuhusu kesi yoyote binafsi au habari zaidi zinazohusiana na kazi ya ofisi ya Haki za Mteja. Ni mwenyekiti tu anayeweza kukataa maombi.

Ofisi ya Haki za Mteja inapatikana kwenye ofisi ya usimamizi ya Huduma za Watoto za Kaunti ya Franklin.

**Barua:**
855 W. Mound Street, Columbus, Ohio 43223
**Email:** cro@fccs.us
**Phone:** 614.275.2621
**Fax:** 614.275.2755



### Kukata Rufaa

Rufaa **inaweza** kukatwa na mtu ambaye shirika limemdhibitisha au kuonyesha kuwa amedhulumu na kumtelekeza mtoto baada ya uchunguzi. Ni mshukiwa pekee (mlalamishi) anaweza kuwasilisha malalamishi ya mtazamo wa ripoti. Mlalamishi lazima awasilishe kesi yake **kwa siku thelathini** baada ya barua ya matokeo ya mtazamo. Hakuna rufaa inaweza kuendelea mpaka kesi zote katika korti la uhaini au la watoto zinazohusiana na matokeo ya uchunguzi zikamilishwe. Kesi zote zinazohusiana na uchunguzi zikikamilika, mlalamishi ataijulisha ofisi **kwa siku thelathini** baada ya uamuzi wa kesi zile.

1. Punde tu ofisi ya Haki za Mteja ikipokea na kuidhinisha maombi ya kukata rufaa, yatatumwa kwa mkurugenzi wa Usajili na idara ya Uchunguzi. Mlalamishi atazungumziwa ili apange siku ya kuwasilisha kesi yake kwa msimamizi wa usajili. Mlalamishi lazima awepo kwa muda wa siku thelathini baada ya kukata rufaa. Mlalamishi anaweza kuleta wakili na mashahidi wanaoweza kutoa habari ifaayo. Barua ya majibu iliyoa-//ndikwa itatumiwa mlalamishi na msimamizi wa Usajili kwa siku thelathini.

2. Ikiwa lile jibu la usimamizi halijasuluhisha rufaa, mlalamishi atawasiliana na ofisi ya Haki za Mteja **kwa siku thelathini** za kupokea jibu hilo la kuomba usikilizwaji wa rufaa. Rufaa itatumwa kwa afisa msikilizi wa usimamizi. Afisa msikilizi hahusiki moja kwa moja katika uchunguzi au uidhinishaji wa msimamo wa kesi. Maombi yakishatumwa, mlalamishi lazima awepo ili kukutana katika siku thelathini. Mlalamishi ni lazima aeleze ofisi kimbele kuhusu marekebisho yoyote maalum yanayohitajika. Mlalamishi anaweza kuleta wakili na mashahidi ambao wanaweza kutoa ushuhuda unaofaa. Kikao kitapangiwa **kwa siku thelathini** baada ya kupokelewa na Ofisi. Vikao vitapangiwa saa moja na vitarekodiwa. Pande zote zitakazoshuhudia zitalishwa kiapo. Afisa msikilizi atapeana ripoti iliyoandikwa **kwa siku thelathini** baada ya vikao. Uamuzi wa afisa msikilizi ni wa mwisho katika Huduma za watoto za Franklin County.

***TAMBUA:*** *Hivi sivyo vikao vya kisheria na kwa hivyo, sheria za ushahidi hazifanyi kazi. Rekodi ya uchunguzi ya Huduma za Watoto inasalia siri kwa sheria na haitatolewa au kupewa mlalamishi kabla, wakati wa au baada ya vikao.*

## Haki zangu zimelindwa zaidi kivipi?

### Kuwasilisha Lalama

Wazazi, waangalizi, walezi halali, walezi wa ukoo,waliotuma maombi au watoaji wa mipango iliyoidhinishwa na kusimamiwa na watu wazima, na watoto walioshirikiana na shirika kwa kusudi lolote linalohusiana na kazi ya shirika itakuwa na haki ya kuwasilisha malalamishi yao kuhusu ushirikiano huo. Kusuluhisha lalama au tatizo kunaweza kuchukua hali tofauti: kufanya kazi na timu ya huduma, mkurugenzi msaidizi; au kupitia lalama- ya awali. Ikiwa matatizo yako hayajatatuliwa kupitia vifaa hivi, lalama linawza kuwasilishwa.

Lalama **ni lalamishi rasmi** kuhusu huduma au ukosefu wake. Kuwasilisha lalama lazima kuwe katika wakati ufaao. Lalama zinaweza kuwasilishwa sio zaidi ya siku thelathini baada ya tukio, au kutambua tukio.

1. Punde tu ofisi ya Haki za Mteja inapokea na kuidhinisha ombi la lalama, itatumwa kwa mkurugenzi wa idara inayofaa. Mwakilishi kutoka ofisi ya Haki za Mteja anaweza kuhudhuria mojawapo ya mikutano yoyote kufuatia ombi la mlalamishi au msimamzi wa idara. Ni lazima ukutane na mkurugenzi na kujadili lalamishi **kwa siku thelathini** tangu kuwasilisha lalama. Mkurugenzi atawasiliana nawe ili mpange siku ya mkutano. Majibu ya mkurugenzi yaliyoandikwa yanafaa kukufikia **kwa siku thelathini** baada ya kupokea lalama yako.

2. Ikiwa majibu ya mkurugenzi hayaridhishi, wasiliana na ofisi ya Haki za Mteja **kwa siku thelathini** baada ya kupokea jibu hilo. Lalama yako itawasilishwa kwa Naibu Mkurugenzi au mtu aliyeteuliwa. Punde tu lalama hii ikifika hapa, unafa kukutana na kujadiliana na Naibu Mkurugenzi au mteule **kwa siku thelathini**. Naibu Mkurugenzi au mteule atawasiliana nawe ili kupanga wakati wa mkutano. Majibu ya Naibu Mkurugenzi yaliyoandikwa yatatumwa kwako **kwa siku thelathini** baada kupokea lalamishi lako.

3. Ikiwa jibu la Naibu Mkurugenzi au Mteule halikuridhishi wasiliana na ofisi ya Haki za Mteja **kwa siku thelathini** baada ya hilo jibu. Lalamishi lako litawasilishwa kwa Mkurugenzi wa Huduma za Watoto wa Franklin County. Lalamishi likishawasilishwa, ni lazima ukutane na kujadiliana na Mkurugenzi Mtendaji **kwa siku thelathini**. Mkurugenzi Mtendaji atawasiliana nawe ili mpange wakati wa mkutano. Jibu lililoandikwa la Mkurugenzi Mtendaji linafaa kukufikia **kwa siku thelathini** baada ya kuwasilisha lalama yako. Uamuzi wa Mkurugenzi Mtendaji ni suluhisho la mwisho katika Huduma za Watoto za Franklin County.



**Bodi ya Huduma za Watoto ya Franklin Kaunti imeamua kuwa watoto na watu wazima ambao ni wateja wa Hili Shirika watakuwa na haki ya:**

1. Huduma za utafsiri, bila malipo kwa mteja, wakati wowote anapoombwa kumsaidia mteja katika shughuli zozote na wahudumu wa Huduma za Watoto, ikiwemo mikutano yote, mipango ya kesi na ushirikiano na Wafanyikazi wa Shirika;
2. Kuhudumiwa kwa njia inayoheshimu mila huku ikizingatiana kuheshimu uhuru, na siri za watu;
3. Huduma kwa njia isiyo na masharti mengi,na ya kibinadamu. Hii imeelezwa katika sheria za Ohio na taratibu katika mpango wa kesi/huduma;
4. Kuratibu rekodi ya kesi yao mradi tu sheria haikatazi haya. Maombi ya habari zozote yaweza kukatazwa ikiwa habari hiyo maisha ya mtu yeyote. Maombi yote ya kupata rekodi za kesi lazima yawe yameandikwa. Watu wanaotaka habari lazima wapeane picha ya kuwatambulisha kabla ya kupata habari za rekodi ya kesi. Ikiwa kuna habari zilizokatazwa na sheria au zingemweka mtu yeyote katika hatari kwenye rekodi, itaondolewa kabla ya kuipata.

    **Ikiwa kesi yako** imefunguliwa kurugenzi wa eneo hilo anawajibika kujibu maombi ya kupata rekodi. Wateja wanaweza kuangalia rekodi yao kwenye ofisi ya FCCS katika uwepo wa wafanyikazi wetu.

    **Kesi yako ikifungwa** tafadhali wasiliana na idara ya sheria kwa 614-275-2584. Habari zinazopeanwa kwa watu wanaoziomba kwa kesi zilizofungwa zitatumwa moja kwa moja kwa mwombaji.

Uamuzi wa kumnyima mteja apate rekodi utaandikwa na upewe kwenye barua.

5. Kuingiza usemi wowote kwa rekodi zao za kesi na kuratibisha usemi wowote uliopeanwa na wahudumu wa Shirika kwa kujibu ule usemi wa mteja;
6. Kuwa na fursa ya kushiriki katika uundaji wa mpango wa kesi na marekebisho ya mpango wa kesi, na wa huduma zilizopendekezwa au zilizopo,matibabu au tiba;afya ya kimwili na kiakili, na mahitaji ya kijamii, na hiyo inaeleza uwepo, ufaaji , na utoshaji wa huduma zinazopeanwa moja kwa moja au kwa rufaa;
7. Kubali au kataa huduma yoyote, au tiba baada ya kuelezwa kikamilifu madhara yanayotarajiwa kutokana na kukubali au kukataa huko isipokuwa uwe umeamrishwa kushiriki katika huduma na amri ya korti ya moja kwa moja au kesi /mpango wa huduma uliochapishwa na korti ya eneo linalofaa. Mzazi au mlezi halali anaweza kukubali au kukataa huduma yoyote, matibabu, au tibu kwa niaba ya mteja mdogo isipokuwa awe ameamrishwa kushiriki kwa huduma na amri ya korti ya moja kwa moja/mpango wa huduma uliochapishwa na korti ya eneo linalofaa.

8. Kesi /mpango wa huduma wa kisasa, ulioandikwa wa kibinafsi unaoangazia usalama wa mtoto,
9. Kuhusika kabisa katika maandalizi, uratibu wa muda kwa muda, na tathmini zaidi ya kesi/mpango wa huduma;
10. Uhuru kutokana na matibabu mengi yasiyofaa ;
11. Uhuru kutokana na kutengwa kusikofaa;
12. Julishwa kuhusu na kukataana na harakati hatari ya kimatibabu;
13. Shiriki katika huduma za shirika zilizopo na zinazofaa , bila kujali kukataliwa kwa huduma moja au zaidi, matibabu, au tiba au bila kujali kukomeshwa kwa matibabu ya awali katika huduma hiyo au nyingine, isipokuwa kuwe na haja maalum na inayofaa ambayo inajumulisha na/inahitaji  kuhusika kwa mteja katika huduma nyingine. Hitaji hili litaelezwa mteja na liandikwe katika kesi ya mteja/mpango wa huduma;
14. Pata fursa ya kushauriana na wataalamu huru wa matibabu au sheria kwa malipo yako mwenyewe;
15. Usiri katka mipaka ya sheria za Ohio au za kitaifa, amri za korti, au kesi iliyochapishwa/mpango wa huduma. Mtu yeyote aliye na uwezo wa kisheria wa kukubalisha utoaji wa habari kuhusu mteja wa Shirika anaweza kufanya hivyo kulingana na sheria za Ohio na za kitaifa;
16. Kuelezwa awali ya sababu ya kuachishwa//huduma na kuhusishwa katika kupanga;
17. Pata maelezo kuhusu sababu  za kunyimwa huduma;
18. Usitengwe katika utoaji wa huduma kwa misingi ya mila, rangi, jinsia, umri, dini, rangi, msimamo wa kijinsia, ulemavu wa kimwili au kiakili, taifa, kiwango cha mapato, au msimamo wa kisiasa;
19. Jua gharama ya huduma;
20. Elezwa kikamilifu kuhusu haki zote;
21. Tekeleza haki zozote na zote bila vikwazo vyovyote , pamoja na kupata huduma, ambayo haifai kuafikianwa;
22. Jaza lalama; na
23. Uwe na maagizo ya sauti na yaliyoandikwa ya kujaza lalama.
24. Saidia kupata ripoti sahihi, ikiwa una miaka 16 au zaidi na kwenye makao ya lile shirika

### Kuhusu watoto tunaowaangalia

Wafanyikazi wa Huduma za Watoto, wazazi walezi, na wazazi wa kutwaa, na watoto kabla ya kutwaliwa, wanafunzwa jinsi ya kujiendesha katika tabia zisizodhibitika. Wafanyikazi na walezi hawatatumia  mikakati yoyote ya kudhibiti tabia ikiwemo:  kuzuiwa au kutengwa kimwili, kimuundo au kikemikali au hata kutengwa kwa kufungiwa.



### Wafanyikazi wa Huduma za Watoto, wazazi walezi, na wazazi wa kutwaa wakiwa na watoto kabla ya kutwaliwa hawata:

**1.** Kagua au kufungua barua yoyote inayoingia au kutoka ya watoto walio katika uangalizi wa Shirika isipokuwa:

**a.** Inashukiwa kuwa na vitu au vifaa haramu , hatari  au visivyoruhusiwa, ambapo barua inaweza kufunguliwa kwenye uwepo wa mtu aliyeteuliwa,
**b.** Kupokea au kutuma barua iliyofungwa imeelezwa katika mpango wa huduma usiohusisha barua pepe, au
**c.** Kupokea au kutuma barua kwa watu maalum ni tishio kubwa kwa usalama wa mtoto au wazazi walezi au kinyume na mahitaji ya yule mtoto na wale watu na sababu za ukaguzi huu wa barua umeandikwa kwenye rekodi ya kesi.

**2.** Zuia haki za watoto walio katika uangalizi wa Shirika wa kuwa na mazungumzo ya kisiri ya simu isipokuwa kuzuia kwenyewe ni:

**a.** Kulingana na maelezo kwenye mpango wa huduma unaohusiana na usalama wa mtoto , wazazi walezi au wahudumu , au ni ya manufaa kwa mtoto, na
**b**. Imeidhinishwa kimbele na kuratibiwa kila mwezi na Mkurugenzi wa eneo au msaidizi wake au mtu aliyeteuliwa,
**c.** Inasasishwa kila wiki na yule Msimamizi wa yule mfanyikazi wa Kesi aliyejukumiwa mtoto,na
**d.** Idhini ile na sasisho zimeandikwa katika ile rekodi ya kesi,
**e.** Au inafuatilia amri maalum ya korti.

Ofisi ya Haki za Mteja inaweza kusaidia katika kujaza lalama ikiwa hauridhiki na huduma. naweza kujaza lalama **sio baada siku thelathini baada ya tukio, au kugundua tukio**. uwasilisha lalama wasiliana na ofisi ya Haki za Mteja (tazama ukurasa 8)

Ofisi ya Haki za Mteja inaweza pia kusaidia katika kukata rufaa ya matokeo ya uchunguzi. Rufaa inafaa kukatwa **kwa muda wa siku thelathini  baada ya kupata matokeo ya uchunguzi.** Ili kukata rufaa ya usimamizi, wasiliana na ofisi ya Haki za Mteja (ona ukurasa 8)

Kwa zile kesi zinazoshughulikiwa na mmojawapo ya mashirika ya ulezi, Permanent Family Solutions Network (PFSN) au National Youth Advocate Program (NYAP), mashirika yanayotoa huduma za ulinzi moja kwa moja kwa familia na watoto, yana taratibu zao za kushughulikia lalama na maswala nyeti. Unashauriwa kutatua shida yako na mhudumu wa kesi au msimamizi. Ikiwa hautaweza kufanya hivyo, tafadhali wasiliana na Afisa wa Haki za Mteja kwa  shirika linaloshughulikia kesi yako.